TANGAZO LA SERIKALI NA 331 LA TAREHE 20/07/2017

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA(MAMLAKA ZA MIJI)

(SURA 288)

_____

SHERIA NDOGO

_____

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89)

_____

SHERIA NDOGO ZA (USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA UVUVI KWENYE MIALO) (BMU) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI ZA MWAKA 2018

Jina la sheria na muda wa kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi kwenye Mialo (BMU) za Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni) za Mwaka, 2018, na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali

Eneo la kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo.

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"BMU" maana yake ni (Beach Management Unit) yaani kikundi cha usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwenye mialo.

"Chombo cha usafiri majini" maana yake ni mtumbwi wa injini au kasi.

"Kamati" maana yake ni kamati ya BMU au mjumbe yeyote wa BMU.

"Kituo" maana yake ni eneo maalum lililotengwa kwa ajili ya BMU kuendesha shughuli zake na wavuvi kushushia samaki wanapotoka kuvua.

"Mwalo" maana yake ni sehemu ya kando kando ya bahari ambayo imetengwa kwa ajili ya shughuli za uvuvi na usimamizi wa BMU katika shughuli za uvuvi.

"Nyavu" maana yake ni nyavu za makila (gillnets) zenye macho yenye ukubwa wa nchi 5,6 na kuendelea.

"Ndoano" maana yake ni ndoano za saizi na 7,8, 9 na 10 tu zinazoruhusiwa kisheria kuopolea samaki.

"Rasilimali za uvuvi maana yake ni mazao yote yatokanayo na shughuli za uvuvi.

"Udhibiti wa ubora wa samaki" maana yake ni uhakiki na uzingatiaji wa ubora wa samaki na vyombo au vifaa vinavyotumika kubebea samaki kabla ya kwenda viwandani kuchakatwa.

"Uongozi" maana yake ni uongozi wa BMU katika mwalo husika.

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi; kikundi cha watu, kampuni au shirika ambalo litakuwa limepewa mamlaka na Halmashauri kukusanya ushuru na kusimamia Sheria Ndogo hizi kwa mada ya Halmashauri.

"Zana za uvuvi" maana yake ni nyavu za makila zenye macho ya ukubwa wa inchi 5, 6 na kuendelea.

Usimamizi wa shughuli za uvuvi.

4. Shughuli zote zinazofanywa na zinazotokana na rasilimali za uvuvi zilizo katika eneo la Halmashauri zitafanywa chini ya Usimamizi wa Halmashauri.

Muundo wa BMU.

5. Kutakuwa na baraza la BMU ambalo litakuwa na muundo ufuatao:-

1. Kutakuwa na Kamati Tendaji yenye wajumbe kumi na tano, wakiwemo Mwenyekiti, Katibu, Mweka Hazina, mtunza bohari, mzee maarufu pamoja na wajumbe kumi. Kamati hii itakuwa na jukumu la kusimamia shughuli zote za Kikundi.
2. Kutakuwa na Kamati ya Fedha na mipango ambayo itakuwa na wajumbe watano ambapo kutakuwa na Mwenyekiti na katibu na wajumbe watatu.
3. Kamati iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 5 (2) pia itakuwa na wajibu wa kupanga mipango ya kuendesha shughuli za kikundi pamoja na kusaidia kukusanya mapato yatokanayo na shughuli za uvuvi kwa idhini ya Halmashauri
4. Kutakuwa na Kamati ya doria ambayo itakuwa na wajumbe watano wakiwemo Mwenyekiti na Katibu. Itakuwa na wajibu wa kufanya doria kwa kusaidia Halmashauri katika utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.
5. Kutakuwa na Kamati ya Takwimu na taarifa ambayo itakuwa na wajumbe watano wakiwemo Mwenyekiti na katibu na itakuwa na wajibu wa kukusanya takwimu za mazao mbalimbali ya uvuvi kwa kushirkiana na Halmashauri.

Usajili wa wavuvi

6. Kutakuwa na orodha ya wavuvi wote katika BMU ambapo kila mvuvi atasajiliwa kabla ya kuanza kazi akionyesha kuwa yeye ni mwenye mali au ni Mwajiriwa katika mtumbwi.

Maegesho ya

7. Mitumbwi yote ya kukusanyia samaki au kusafirisha mizigo au abiria itaegeshwa umbali wa mita kumi

mitumbwi

kutoka kwenye uzio.

Kuhudhuria Vikao

8. Kila mvuvi au mwanachama wa BMU atalazimika kuhudhuria vikao vya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wavuvi au Kamati ya Mazingira pale vikao vitakapoitishwa na Kamati hizo.

Vyoo vya umaa

9. Kutakuwa na Vyoo vya Umma vitakavyo jengwa na kusimamiwa na Halmashauri katika maeneo ya mwalo na vitaendeshwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Sheria za Afya.

Uhakiki wa ubora wa Samaki

10. Magari yote yatakayobeba samaki yatakuwa ni magari maalum yenye cheti cha samaki kutoka kwa Afisa Mfawidhi wa udhibiti wa ubora wa samaki na viwango ambayo;-

(a) yatatakiwa kuwa na nembo ya samaki ubavuni na picha ya samaki;

(b) hayatatakiwa kuwa na vumbi au kutu;

(c) yatatakiwa kuwa na milango iliyotengenezwa kwa kutumia vifaa vinavyo kubalika katika viwango vya ubora.

Makosa

11. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo :-

a. atafanya shughuli za uvuvi bila kibali maalum kutoka ya Halmashauri;

b. atavua samaki kwa kutumia sumu, mabomu, kemikali au nyavu zisizoruhusiwa au kuvua samaki katika maeneo yasiyoruhusiwa;

c. atavua samaki kwa kutumia mitego ya mtando (Ring nets) katika maeneo

yenye maji madogo chini ya kina cha mita arobaini (40m);

d. atachafua mazingira kwa kutupa takataka au kujisaidia katika maeneo ya fukwe, bandari au masoko;

e. atavuna au kukata miti ya mikoko bila kibali maalum;

f. atajisaidia baharini,mtoni na bwawani au kutotumia vyoo vilivyotengezwa katika maeneo ya makambi;

g. atavua pweza chini ya uzito wa gramu 500;

h. atafanya shughuli za uvuvi katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mazalia ya samaki na viumbe wengine wa baharini,mtoni na mabwawa;

i. atauza au kukausha samaki katika maeneo machafu, au mchangani;

j. atauza au kununua samaki katika maji au baharini au sehemu nyingine yeyote isiyotengwa kama soko la samaki;

k. atamzuia Afisa yeyote wa Halmashauri, au mjumbe wa BMU kutekeleza majukumu yake halali ya usimamizi.

Adhabu

12. Mtu yeyote atakayenkwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (Tshs. 50,000) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au adhabu zote

kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

13. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini ya kiasi kisichopungua shilingi za kitanzania elfu thelathini (30,000/=) endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe na kujaza fomu maalumu iliyoainishwa kwenye Jedwali la Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI

KUFIFILISHA KOSA

(Chini ya kifungu cha 14)

Mimi ……wa S.L.P…….. nakiri KWA HIYARI YANGU MWENYEWE mbele ya……..ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya manispaa ya Kigamboni kwamba mnamo tarehe……ya Mwezi….Mwaka……nilitenda kosa la kwenda kinyume na masharti ya kifungu cha ……..cha Sheria Ndogo za (Udhibiti na Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi kwenye Mialo (BMU)) za Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni) za Mwaka, 2018.

Kwa mamlaka aliyopewa na Mkurugenzi wa Halmashauri. Niko tayari kulipa faini ya kiasi cha Shillingi……....

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIYARI YANGU KWA KADIRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……..ya mwezi……mwaka……

Jina……...……...Saini…….....

Mbele ya:

Jina……...…….

Saini…….….....

Wadhifa……

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa Kigamboni imebandikwa kwenye hizi Kanuni za Kudumu kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 31 Januari, 2018 mbele ya:-

L.S

STEPHEN E. KATEMBA
Mkurugenzi,
Halmashauri ya Manispaa Kigamboni.

MAABAD SULEIMAN HOJA
Mstahiki Meya
Halmashauri ya Manispaa Kigamboni.

NAKUBALI

DODOMA,
07 Juni, 2018

MHE. SELEMANI S. JAFO (MB)
Waziri Wa Nchi/Or Tamisemi.